

JINA.....NAMBA YAKO.....

TAREHE.....

SHULE..... SAHIHI YA

MTAHINIWA.....

102/3

KISWAHILI

KARATASI YA TATU

FASIHI YA KISWAHILI

MUDA: Saa 2½

MUUNGANO WA SHULE MBALIMBALI MTIHANI WA KUJITATHIMINI JULAI / AGOSTI 2010

102/3

KISWAHILI

FASIHI YA KISWAHILI

KARATASI YA 3

MAAGIZO

- ❖ *Jibu maswali manne pekee*
- ❖ *Swali la kwanza ni la lazima*
- ❖ *Maswali hayo mengine matatu yachaguliwe kutoka sehemu nne zilizobaki yaani: Riwaya, Tamthilia, Hadithi fupi na Ushairi.*
- ❖ *Usijibu maswali mawili kutoka sehemu moja.*
- ❖ *Watahiniwa ni lazima wahakikishe kuwa kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.*

1. (LAZIMA)

FASIHI SIMULIZI

i) Eleza maana ya nyimbo (alama 2)

.....
.....
.....

ii) Taja vigezo vinne muhimu vinavyotumiwa kuzipa majina aina mbalimbali za nyimbo. (alama 8)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

iii) Eleza muundo wa nyimbo kwa jumla. (alama 5)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

iv) Fafanua umuhimu wa nyimbo za tahili katika jamii. (alama 5)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

2. RIWAYA: UTENGANO: S.A Mohamed

- (i) Wanawake wamezinduka na kuanza kutetea haki zao. Fafanua dhana hii ukirejelea riwaya ya utengano. (alama 20)

AU

- (ii) “Mabibi na mabwana.....Maksuudi Kambe si mgeni kwenu. Katika umri wake huu alio nao hajabadilika.”

- a) Fafanua mkutadha wa dondoo hili. (alama 4)
b) Thibitisha kuwa madai haya ni kinaya. (alama 16)

3. HADITHI FUPI: MAYAI WAZIRI WA MARADHI NA HADITHI NYINGINE:

K.W Wamitila

Jiinsia ya kiume ndicho kiini cha maovu yanayoikumba jamii. Thibitisha kauli hii ukirejelea hadithi zifuatazo.

- (i) Mayai waziri wa maradhi
(ii) Siku ya mganga

AU

4. NDIRI ZA MAUTI: TIMOTHY M. AREGE

“.....Moyoni alihisi ndimi za aina yake zikimwunguza. Ndimi za mauti.”

- a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Fafanua maana ya “Ndimi za mauti.” Kwa mujibu wa hadithi hii.(alama 6)
c) Thibitisha madai kuwa mkasa unaorejelewa katika hadithi hii ulitokana na kutowajibika. (alama 10)

5. KIFO KISIMANI: Kithaka wa Mberia

“Msimamo wangu hautokani na uwoga. Umetokana na kuthamini maisha ya binadamu.”

- a) Liweke dondoo hili katika muktadha wake. (alama 4)
b) Ni vipi ambavyo maisha ya binadamu hayakuthaminiwa? (alama 8)
c) Ni mbinu zipi zilizotumiwa na raia kuuangamiza uongozi wa kiimla katika Butangi? (alama 8)

6. USHAIRI

Soma shairi hili kisha ujibu maswali yanayofuata

1. Dunia kitu dhaifu, si ya mtu kunyetea,
Usione ufanifu, na furaha kila njia,
Kumbuka na uvunjifu, kama ndwele hukujia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

2. Anasa usiandame, kwa pupa kuzipapia,
Heri moyo fanye tume, uche na kuzikimbia,
Hakuna mume wa dume, na wala hatatokea,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

3. Wako wapi mashujaa, wenye nguvu kila njia,
Ziliwafika nazaa, wakabaki kujutia,
Ndunia ina hadaa, yataka kuzingatia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

4. Kam kam mahuluki, viumbe vyake jalia,
Walokuwa na maluki, bora za kujivunia,
Muda wakitahamaki, iliwatupa dunia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

5. Fikiri zao sharafu, walizo wakitumia,
Penye unasi alifu, wanenalo maridhia,
Mwisho wayo madhaifu, na majina kupotea,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

6. Walishushwa ghorofani, mapambo na mazulia,
Wakawachia wandani, na mali zilizosalia,
Wameshia kaburini, udongo kuwafukia,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

7. Naturudi kwa manani, tutubu zetu hatia,
Kwa baraka za Amini, Mola tatughofiria,
Tutafuzu duniani, mema na ahera pia,

Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

8. Turudipo kwa Jalali, tukayawacha mabaya,
Kila sada tutanali, na shari kutwepushiya,
Tutapata na uvuli, ahera kujifichiya,
Tagaa bovu dunia, ndu yangu silewelewe.

MASWALI

- a) Pendekeza anwani mwafaka kwa shairi hili (alama 1)

.....
.....

- b) Taja na ufafanue mifano yoyote minne ambayo mshairi ametumia kuisisitiza ujumbe wake. (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

- c) Kulingana na mshairi, ni mambo gani yanayopaswa kuepukwa? (alama 4)

.....
.....
.....
.....

- d) Taja na ueleze mbinu mbili za kifasihi zilizotumika katika shairi hili. (alama 2)

.....
.....
.....
.....

- e) Eleza muundo wa ubeti wa tatu wa shairi hili ukizingatia mizani na vina (alama 2)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

f) Andika ubeti wa sita katika lugha nathari. (alama 4)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

g) Eleza maana ya maneno yafutayo kama yalivyotumika katika shairi.

i) Kam kam

.....
.....

ii) Tutaghofiria

.....
.....

iii) Madhaifu

.....
.....

(alama 3)